

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HALMASHAURI YA MJI WA KASULU.

SHULE YA SEKONDARI
NYANTARE
S.L.P 475,
KASULU.
11/12/2020

SIMU: 0753184572
0783954072
Email: nyantaress2020@gmail.com

Kumb Na. NTR.JOIN/KTC/2020/VOL. 02

MWANAFUNZI _____

S.L.P _____

KASULU.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYANTARE HALMASHAURI YA MJI WA KASULU MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. **Hongera sana.** Shule ya sekondari Nyantare ipo umbali wa kilometa sita kutoka ofisi za Halmashauri ya mji wa Kasulu.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021 na muhula wa kwanza unanza tarehe 11/01/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE.

(a) WAVULANA.

- (i) Suruali mbili za **BILINGANYA** zenye “cerebration” mifuko mitatu, mfuko wa nyuma usiwe wa kubandikwa , pia tai mbili.

NB: Unashauriwa kushona suruali zenye heshima (Suruali zinazobana/Modo hazikubaliki).

- (ii) Shati mbili nyeupe mpya mikono mifupi. (Polister cotton)
(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
(iv) Ti-shirt ya rangi ya **ZAMBARAU** yenye nembo ya shule.
(v) Soksi nyeusi jozi mbili
(vi) Sweta rangi ya **ZAMBARAU.**
(vii) Raba kwa ajili ya michezo.

(b) WASICHANA

- (i) Sketi mbili rangi ya **BILINGANYA** (kitambaa cha suti) zenye rinda nane (8) ndefu ya kufika kwenye **jicho la mguu** na tai zake mbili. (kama hujaelewa njoo uone mfano shuleni)
- (ii) Vazi la Hijabu, linatakiwa la kitambaa kizito (cheupe) lisiloonesha maumbile.
- (iii) Shati mbili nyeupe mpya mikono mifupi. (Polister cotton)
- (iv) Viatu vyeusi pea mbili vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
- (v) Ti-shirt ya rangi ya **ZAMBARAU** yenye nembo ya shule.
- (vi) Soksi nyeupe jozi mbili
- (vii) Raba kwa ajili ya michezo
- (viii) Sweta rangi ya **ZAMBARAU**.

KUMBUKA: Yeboyobo, Ndara na viatu vyovyote visivyoagizwa haviruhusiwi shuleni, ukikamatwa navyo unanyang'anywa na haurudishiwi.

2.2. VIFAA VYA TAALUMA.

- Kila mwanafunzi anashauriwa kuwa na vifaa vya taaluma vifuatavyo:-

- i) Daftari kubwa kumi (10) kuanzia Quire 3.
- ii) Mkebe wa Hisabati
- iii) Kamusi ya kiingereza kwa kingereza
- iv) Kalamu za wino na risasi (penseli) za kutosha.

NB: Vifaa hivi ni kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi.

3.0 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kwa umakini mkubwa sana:-

- (a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima. (**UTORO HAPA KWETU NI MWIKO, KAMWE HAUVUMILIWI**)
- (b) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (g) Kutunza mali za umma.

3.1 **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI
KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ubakaji.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
4. Kupiga au kupigana.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
6. **Utoro wa aina yoyote.**
7. Kuharibu bendera ya Taifa/ kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
9. Kuoja au kuolewa.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi.

KUMBUKA: Kuja na Cheti cha kuzaliwa au Affidavit Form.

4.0 **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA
NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI NI:-**

- (a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali (**HAKIKISHA MWANAO ANAPIMA KIKAMILIFU**). Fomu hiyo iwasilishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, utoro na makosa ya jinai.
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelezo mengine yanayotolewa na shule.


5.0 **TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO
HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.**

**: MTOTO MTORO NA ASIYE NA NIDHAMU KATIKA SHULE HII
HATUMUHITAJI KABISA.**

NB: Kutakuwa na kikao cha kwanza cha wazazi wote wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kitakachofanyika tarehe **29/12/2020** na kikao cha pili kitafanyika tarehe **28/01/2021** saa 3:00 asubuhi chenye lengo la kutoa maelekezo juu ya taratibu na kanuni za shule.

Kwa mawasiliano zaidi piga 0753184572/0783954072.

“KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYANTARE”



.....
MICHAEL KAZEMBE BENEZETH
MKUU WA SHULE.

THE HEADMASTER
NYANTARE SECONDARY SCHOOL
KASULU TOWN COUNCIL

AFFIDAVITY FORM

(To be filled by Tanzanians only).

I Tanzania, do here make out and state I
am the father / mother / relative of
was born at
on the day of 20
and that I was present at /shortly after the birth of the said
that had personal and direct knowledge of the said
on account of
.....
.....

(Describe the circumstances of such personal and direct knowledge) of
said Was a Girl/Boy.

Signed
shown at this day
Day of 200
Before me
Qualification
Address
Signature

(Official stamp or seal)